**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

**Toleo: 1444/08 H** **Jumapili, 27 Sha'aban 1444 H** **19/03/2023 M**

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

# Ujumbe kutoka Hizb ut Tahrir / Kenya Wakutana na Wanazuoni Mashuhuri wa Kiislamu

**(Imetafsiriwa)**

Ujumbe kutoka Hizb ut Tahrir/Kenya ukiongozwa na Ustadh Mahd Ali - Mkuu wa Kamati Kuu ya Mawasiliano ya Hizb ut Tahrir nchini Kenya akifuatana na Ustadh Yusuf Ghasani na Ali Mwangi ambao wote ni wanachama wa Hizb ut Tahrir, walikutana na viongozi kadhaa mashuhuri wa Kiislamu walioko Mji Mkuu wa Kenya Nairobi miongoni mwao:

**Naibu Kadhi Mkuu wa Kenya Sheikh Sukyan Hassan Omar**

**Sheikh Juma Amir Imam Msaidizi wa Msikiti wa Jamia, Nairobi**

**Daktari Mbarak Ahmed Awes Imam Msikiti wa Al-Hudaa South B Nairobi**

Ujumbe huo wa Hizb ulipokelewa kwa mapokezi mazuri. Mkuu wa ujumbe huo, Ustadh Mahd Ali aliweza kushiriki majadiliano yenye maana na viongozi hao kuhusu LGBT na Da'wah ya Kiislamu kwa jumla. Aliwapa nakala ya kitabu, *Khilafah*, chapisho la Hizb ut Tahrir kinachoelezea ufaradhi juu ya Waislamu wa kusimamisha tena Khilafah.

Twamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azifungue nyoyo za Maulamaa wafanye kazi na Hizb ut Tahrir katika kufikia lengo la kurudisha mfumo kamili wa maisha wa Kiislamu kwa kusimamisha Khilafah Rashida ya pili kwa Njia ya Utume.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir**
**Kenya**

**Simu**: +254 707458907
**Pepe:** mediarep@hizb.or.ke
**Tovuti ya Hizb ut Tahrir Kenya:**
www.hizb.or.ke

**Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:**
www.hizb-ut-tahrir.org
**Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:**
www.hizb-ut-tahrir.info